HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE AKIONGEA NA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KATIKA SHULE YA SEKONDARI JANGWANI WILAYA YA ILALA, MKOANI DAR ES SALAAM,

TAREHE 28 APRILI, 2010.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu William Lukuvi

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Bw. Leonidas Gama

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ndugu John Guninita

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Zarina Madabida

Mheshimiwa Mbunge Jimbo la Ilala ,Ndugu Musa Zungu

Wabunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Janet Masaburi na Bibi Janet Kahama

Waheshimiwa Madiwani

Viongozi wote wa Chama na Serikali,

Walimu na wanafunzi, Mabibi na Mabwana,

Habari za mchana!

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kujumuika kwa pamoja wakati huu hapa Shule ya Sekondari Jangwani. Nakumbuka nilikuja hapa tarehe 28 Februari, mwaka huu kwa ajili ya kuwaona wanafunzi wenzenu wa Shule yetu ya Sekondari WAMA-Nakayama ambao mliwapokea. Leo hii, kama nilivyokuwa nimewaahidi, nimefika tena kwa ajili ya kuzungumza nanyi wanafunzi wa jangwani na wanafunzi wengine wa shule za Sekondari na Msingi.

Ndugu Viongozi, Walimu, na wanafunzi

Kabla sijaendelea naomba kuwasilisha ujumbe kutoka kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu. Jakaya Mrisho Kikwete. Anawasalimu na anawatakia mafanikio mema katika masomo yenu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Wapendwa wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Mimi kama M/kiti wa WAMA, mama na pia Mlezi nimefanya ziara kama hii katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu, na leo hii nipo hapa Jangwani ndani ya Mkoa wa Dar-Es-Salaam.

Katika ziara hizo nimeweza kukutana na wanafunzi wa kike na kunzungumza nao kuhusu tabia na mienendo mizuri ambayo wanatakiwa waifuate ili kuepuka changamoto zinazoweza kupelekea kukatiza masomo yao.

Japokuwa changamoto za wanafunzi wa kike zinafanana lakini kwa nyie mlioko Dar es salaam, mna changamoto nyingi hasa tukizingatia kuwa jiji hili lina kila aina ya starehe zenye vishawishi vingi. Hivyo inanibidi nizungumze na nyie kwa kina zaidi. Kwani nia ya kufanya hivyo ni kuwasaidia mpate kuelewa kisha kupambanua yapi ni mazuri na yapi ni mabaya (Faida na hasara)

Sio tu uelewa wa kitaaluma, bali pia katika kujiepusha na mitego, vishawishi, na matendo yanayoweza kuwasababishia matatizo.

Wanafunzi hupata vishawishi ambavyo huwapelekea kupoteza umakini, muelekeo na kuwa watoro, kupata ujauzito, maambukizo ya virusi vya UKIMWI, na hatimaye kupoteza kabisa fursa hii adimu na adhimu ya Elimu yako ya sekondari(Na dira ya maisha yako kwa ujumla).

Wapendwa wanafunzi,

Msikubali vishawishi kwani peremende ya dk si sawa na asali ya maisha. Iweje uridhie kuuharibu muundo/mpango wa maisha yako kwa kitu cha mara moja ? Mnapaswa kuviepuka vishawishi na vitendo vyote vinavyoweza kusababisha kuingia kwenye matatizo Licha tu ya kuwa atakayehusika na kosa la kukupa mimba wewe anapaswa kushtakiwa kisheria, lakini kwako wewe

utakayekuwa umebeba hiyo mimba ni jambo la hatari kiafya. Inawezekana usiwe umepata mimba tu, bali pia ukawa umeambukizwa Virusi vya Ukimwi. Kumbukeni haya ninayowaasa ili yawasaidie kuepuka vishawishi vya chipsi-kuku, lifti, simu za mkononi mnavyorubuniwa navyo.

Vishawishi vya namna hii, havina lolote jema katika kukukomboa msichana kielimu, kijamii na kiuchumi.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Napenda nizitambue jitihada na mwamko mkubwa wa kutambua umuhimu wa Elimu kwa ongezeka la shule mpya za sekondari katika Wilaya ya Ilala. Kwa upande wa shule za serikali kuna ongezeko la wastani wa asilimia 84, na kwa upande wa shule za binafsi ongezeko la wastani wa asilimia 53, Kimkoa. Kwa

Wilaya ya Ilala peke yake, kuna ongezeko la asilimia 78 na asilimia 53 kwa maeneo hayo mawili ya umiliki.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, viongozi, Mabibi na Mabwana

Nimefarijika sana na kuwa na matumaini makubwa kwa mwamko huu unaojithibitisha kitakwimu.

Sina Shaka fursa za elimu kwa ujumla, na hasa zile za mtoto wa kike kwa elimu ya sekondari zitaongezeka kwa kiwango kikubwa.

Licha ya changamoto mnazokumbana nazo, nawapongeza sana kwa maendeleo haya ya ujenzi wa shule mliyoyafikia.

Pia napenda niwapongeze kwa namna mlivyopanga mikakati ya kuzikabili changamoto mnazokumbana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na tatizo la upungufu wa walimu, kwa kuwahamishia sekondari walimu wenye diploma na shahada wafundishao

shule za msingi. Mnachukua hatua nzuri na zinazostahili pongezi, kwani itachangia kuboresha elimu mnayoitoa kwa wanafunzi wetu.

Sambamba na hili Mkoa unafanya vizuri sana kitaaluma. Hakikisheni namba yenu inabaki hapo hapo. Kwani hakuna mtu asiyependa kuwa namba 1

Hongereni sana!

Mabibi na Mabwana

Nikiwa kama Mwenyekiti wa Taasisi ya WANAWAKE na MAENDELEO (WAMA), napenda kusema japo kidogo kuhusu azma na shughuli ambazo taasisi hii inajihusisha nazo.

Azma ya WAMA ni kumkomboa mwanamke!. Azma hii ndiyo iliyonisukuma kuanzisha Taasisi ya WAMA ninayoiongoza. Taasisi hii, licha ya kujihusisha na shughuli za uboreshaji afya ya mama na mtoto, pia inajihusisha na uwezeshaji wanawake kiuchumi. Aidha taasisi haiko nyuma katika suala la utoaji wa

fursa za elimu hususan Elimu kwa mtoto wa kike. Pia taasisi hii inashughulikia watoto yatima na waishio katika mazingira.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, viongozi, Mabibi na Mabwana

Wote ni mashahidi juu ya historia ambayo mtoto wa kike imemfikisha hapa. Lakini yaliyopita Si ndwele tugange yaliyopo na yajayo.

Kwa kuwa sasa fursa tumepata basi sisis kama wasichana jukumu letu kubwa ni kusoma kwa bidii sana na tujiamini kwamba sisi tunaweza kwani wote ni binadamu tuna uwezo na akili iliyo kuwa sawa, tofauti ni maumbile tu.

Anachoweza kufanya mtoto wa kiume kitaaluma na mtoto wa kike halikadhalika anaweza. Kuanzia sasa tukate shauri kwamba masomo ya sayansi na hisabati si ya wanaume pekee bali hata sisi tunaweza.

Wapendwa Wanafunzi

Nimalizie kwa kuwapa herufi hizi tatu ambazo zitawahakikishia usalama na ustawi wa maisha yenu nazo ni (JJJ)

Ndugu wananchi

Baada ya kusema hayo, nawashukuru tena viongozi wa Mkoa, Wilaya na wananchi wote kwa ujumla kwa mapokezi yenu mazuri. Nawatakieni kila la heri katika shughuli zenu za ujenzi wa taifa!

Ahsanteni kwa kunisikiliza!